

MKATABA WA UDHAMINI KWA MKOPESHWAJI

(Fomu hii ijazwe na Mdhamini)

Mkataba huu umefanyika leo hii tarehe.....mwezi.....20.....

KATI YA

Ndugu.....namba
(uanachama).....ambaye ni mdhamini wa
Ndugu.....(mkopeshwaji) kwa
upande mmoja.

NA

MALENGO SACCOS LTD ambaye ndiye mkopeshaji kwa upande mwingine.

Kwa kuwa **MALENGO SACCOS LTD** imetoa mkopo kwa
Ndugu.....Mkopopeshwaji.

Na kwa kuwa Nduguambaye ni mdhamini yuko tayari
kumdamini mkopeshwaji.

BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA MAKUBALIANO YAFUATAYO:

Kwamba mdhamini anadhamini ulipajiwa mkopo wa kiasi cha shilingi
..... (Tshs.....) Pamoja na riba yake.
Endapo mkopeshwaji hatalipa mkopo huu, basi mdhamini atawajibika kuulipa pamoja na gharama
ambazo chama kitaingia kutokana na ufuatiliaji wa ulipaji wa mkopo wa mwanachama aliyetajwa hapo
juu.

Kwamba mdhamini anatoa na kuweka kama dhamana Hisa na Akiba zake alizonazo katika chama. Hii
inamaanisha kwamba mkopeshaji anayo haki ya kuchukua amana au akiba ya mdhamini ili kufidia deni
lote analodaiwa mkopeshwaji.

Kwamba dhamana hii itaendelea kuwa na nguvu hadi malipo yote ya mkopo, riba ya kawaida na ya
adhabu pamoja na gharama atakayoingia mkopeshaji katika kufuatilia ulipaji wa mkopo yatakapokuwa
yame fanyika na hati ya kuthibitisha kufanyika kwa malipo hayo kutolewa kwa mkopeshwaji.

Kwamba ikiwa mkopaji aliyetajwa hapo juu atashindwa kulipa malipo na sehemu ya malipo yaliyotajwa katika Mkataba huu mdhamini anaahidi kufanya malipo hayo yote mara tu mkopeshaji atakapomtumia hati ya madai.

Kwamba mdhamini anajua sehemu anapoishi mkopaji, hii ikimaanisha kwamba anajua na anaweza kufika kwenye mtaa na nyumba anapoishi mkopaji kwa sasa, na kama mkopeshaji akihitaji kufika nyumbani kwa mkopaji, mdhamini anaweza na atakuwa tayari kumpeleka hadi nyumbani kwa mkopaji bila tatizo lolote.

Kwamba Mdhamini anatakiwa kufahamu yote yaliyomo kwenye mkataba wa sasa, na kuwa chini ya sheria anawajibika sawa na mkopaji wa mkopo huo ambao yeye ameudhamini. Pia hawezi kujitoa katika udhamini endapo kutatokea marekebisho au kutatokea kuvunjika kwa maelewano au uhusiano kati yake yeye mdhamini na mkopaji

Dhamana hii haitaathiri mkataba mwingine wowote ule ambao mkopeshwaji atakuwa ameingia na chama.

Kwamba mdhamini anathibitisha kuwa amesoma kwa makini na kuelewa vipengele vyote vya dhamana hii na kwamba amekubaliana navyo na ametia saina kwa hiari yake bila kulazimishwa au kushurutishwa na mtu yeyote.

MDHAMINI :

JINA (MDHAMINI).....

SAINI.....

ANUANI.....

.....

TAREHE

MKOPAJI:

JINA:

SAINI.....

ANUANI.....

.....

TAREHE